

wanawake na wanawake.

lata Meru nchini Kenya kuchoma moto hivi karibuni. Eneo hilo limefika Mtandao).

* Wafugaji wapatiwa ng'ombe wa maziwa *



BUSIA

SERIKALI ya kaunti ya Busia imesambaza ng'ombe wa maziwa kwa wafugaji wenye thamani ya jumla ya Sh milioni 24 ili kukabiliana na upungufu wa maziwa katika kaunti hiyo.

Fedha hizo zinatumiwa kununua ng'ombe wa maziwa 244 kwa ajili ya kata 35, ambapo wafugaji katika kata ya Chakol Kaskazini wamepata ng'ombe 40, Burumba 18 Nambale 10 na Maenje

watano.

Gavana wa kaunti hiyo, Sospeter Ojaamong, alisema mradi huo una lengo la kupunguza matatizo ya lishe kwa wananchi kutokana na takwimu za Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo (Kalro) kuonesha kati ya watoto 100 wa umri wa chini ya miaka mitano katika kaunti hiyo, 26 26 wanasumbuliwa na utapiamlo.

"Lengo ni kuboresha uzalishaji wa maziwa utakaozeshesha kuinua uchumi wa watu kupitia mauzo ya

maziwa ya ziada, lakini pia kuweka usalama wa chakula," alisema Ojaamong.

Busia kwa sasa inazalisha lita 82,191 za maziwa kwa siku na takribani lita milioni 27 kwa mwaka, huku ikizalisha lita milioni 27 kwa mwaka, wakati mahitaji ni lita 60,000 kwa mwaka.

Gavana wa Kericho, Paul Chepkwony na Ojaamong wamekubaliana kujadili suala la upungufu wa maziwa kwa wafugaji wa Kericho kuuza bidhaa hiyo Busia.

Waki

KISUMU

W

wagilia wamet mpung moja k umwa nzuri.

Me aji kat Tanui wana kezo nyatt kuuz kati l



(kulia),
apatia

RC aagiza wanaotumia vyandarua kuvua samaki wakamatwe

NA TIGANYA VINCENT, TABORA

MKUU wa Mkoa (RC) wa Tabora, Aggrey Mwanri, amewaagiza viongozi wa vijiji na mitaa, kuwakamata watu wote watakaokutwa wakitumia vyandarua kwa matumizi mengine tofauti na kujikinga na mbu.

Amesema kwamba, matumizi ya vyandarua tofauti na kujikinga na mbu, yanapingana na juhudi za Serikali za kupambana malaria na kusababisha kupoteza nguvu kazi ya Taifa.

Mwanri alitoa maagizo hayo juzi wilayani Kaliua, Mkoa wa Tabora, wakati wa uzinduzi wa kampeni ya Mkoa wa Tabora iitwayo ziro malaria inaanza na mimi.

"Kuna baadhi ya watu wanatumia vyandarua kuvulia samaki katika madimbwi na wengine wanavitumia kuzungushia vifaranga vya kuku visishambuliwe na mwewe.

"Kuna wengine wanavitumia vyandarua hivyo kwa ajili ya kuzungushia bustani za matunda na mboga mboga ili kuzuia wadudu waharibifu.

"Matumizi hayo yote ni kinyume na kujikinga na mbu wa maralia, jambo ambalo siwezi kulivumilia kwa sababu linakwenda kinyume na maagizo ya Serikali ya kupambana na maralia.

"Kwa hiyo, kuanzia sasa, nyinyi viongozi wa vijiji na mitaa, wakamateni wote wanaotumia vyandarua kuvulia samaki na katika matumizi mengine kwani hayo siyo malengo la Serikali," alisema Mwanri.

Awali, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Honoratha Rutatatinisibwa, alisema mwelekeo wa Serikali ni kuhakikisha ifikapo mwaka 2030, ugonjwa wa malaria uwe umetokomezwa.

"Takwimu zinaonyesha kwamba, kiwango cha maambukizi ya ugonjwa wa malaria kwa Mkoa wa Tabora bado ni kikubwa kwani Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua ina asilimia 16.7, Uyui ina asilimia 16.1 na Wilaya ya Sikonge ina asilimia 13.9.

"Wilaya ya Urambo ina asilimia 12.8, Manispaa ya Tabora ina asilimia 8.9, Halmashauri ya Wilaya ya Nzega ina asilimia 8.7, Nzega Mji ina asilimia 6.8 na Wilaya ya Igunga ina asilimia 5.6.

"Kwa hiyo, nguvu zaidi zinahitajika katika kupambana na tatizo la malaria mkoani Tabora kabla hali haijawa mbaya zaidi," alisema Dk. Rutatatinisibwa.

la

ya kazi
kitumia
kufanya
ana.

iachwe
hamini,
enzake
a Babu
izi wa
Nomen
wasi-
a ndoa
Mjini
i Sam-
kutoa
lo vya

ata ya
ili haki
awake
tatua